

Chanjo ya virusi vya korona

– Comirnaty (Pfizer/BioNTech)

Maelezo ukiwa umepokea chanjo hii

Virusi vipya vya korona husababisha maambukizi ya mfumo wa upumuaji. Watu wengi huonyesha dalili ndogo au kutoonyesha dalili zozote, lakini wengine huenda wakawa wagonjwa sana. Watu wazee na wengine ambao tayari wana magonjwa fulani mengine ya msingi wako katika hatari kubwa ya kuugua sana au kufariki. Chanjo ya virusi vya korona inazuia ugonjwa wa COVID-19. Lengo kuu ni kulinda afya na maisha.

Nani anayepaswa kupokea chanjo ya virusi vya korona?

Chanjo za virusi vya korona zinazotolewa kupitia mpango wa kitaifa wa utoaji chanjo zinatolewa kwa watu wanaoishi nchini Norwe. Chanjo hii inatolewa bila malipo na ni hiari yako kuipokea.

Nitapataje chanjo hii?

Angalia tovuti ya manispaa yako ili upate maelezo kuhusu wanaopokea chanjo, jinsi mchakato wa utoaji chanjo unavyopangwa na wakati itakapotolewa.

Mtu anapokea chanjo hii kwa njia gani?

Chanjo hii inadungwa katika sehemu ya juu ya mkono. Kabla ya kuchanjwa, utaulizwa kama wewe ni mgonjwa au hapana na kama umewahi kupata mizio ya chanjo zingine ulizowahi kupokea hapo awali. Kumbuka kusema ikiwa umewahi kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19 au kupokea chanjo ya virusi vya korona hapo awali, ikiwa wewe ni mjamzito, una mizio, unatumia dawa au ikiwa una matatizo mengine ya kiafya. Fuata mwongozo kuhusu idadi ya dozi za kupokea na vipindi vya muda wa kupokea vinavyotumika kwenye kikundi chako. Kituo cha kutoa chanjo kinaweza kukusaidia kuhusu suala hili. Ni muhimu upate dozi kwa wakati ulioratibiwa. Ni jambo la kawaida kuahirisha kupokea chanjo ikiwa una maradhi ya muda mfupi na ukiwa na kiwango cha joto mwilini kinachozidi 38 °C. Baada ya kuchanjwa, utaombwa usubiri katika kituo cha kutoa chanjo kwa angalau dakika 20.

Chanjo hii inafanyaje kazi?

Chanjo hii ina kiungo (messenger RNA) cha miiba iliyo kwenye virusi vya korona. Mwili hutengeneza miiba inayofanana na hii isiyo na madhara, ambayo mfumo wa kinga mwilini unaweza kuitumia ili kujifunza kukabiliana virusi hivyo. Kwa kufanya hivyo, mfumo wa kinga mwilini hujifunza kutambua miiba ya virusi vya korona na unaweza kulinda mwili ikiwa utaambukizwa virusi hivyo. Kiungo cha messenger RNA huvunjwawunjwa mwilini kwa haraka na hakina madhara yoyote kwenye nyenzo ya jenetiki.

Chanjo hii haina virusi vilivyo hai na haisababishi ugonjwa wa COVID-19. Chanjo ya virusi vya korona hutumiwa kuzuia ugonjwa huo. Haiwezi kutibu ugonjwa ambao tayari upo.

Njia hii ya kutengeneza chanjo haijawahi kutumiwa kwa magonjwa ya kuambukizwa kwa binadamu hapo awali, lakini teknolojia hii inajulikana na inatumiwa katika matibabu ya kansa.

Chanjo hii inafanya kazi vizuri kwa njia gani?

Chanjo hii inakulinda dhidi ya ugonjwa unaosababishwa na virusi vipya vya korona. Kiwango cha ulinzi dhidi ya kupata ugonjwa *mkali* ni cha juu baada ya kupokea dozi ya kwanza na ya pili. Unahitaji kupokea dozi mbili ili uimarisha ulinzi dhidi ya *kuambukizwa* virusi vya korona. Bado hatujui kipindi cha kudumu kwa ulinzi. Ikiwa kiwango cha ulinzi kitapungua baada ya muda, huenda ikawa muhimu upokee dozi ya nyongeza. Chanjo haizuii kabisa hali ya kusambazwa zaidi kwa maambukizi. Kwa hivyo, ni muhimu kuendelea kufuata ushauri wa sasa kuhusu kudhibiti maambukizi.

Madhara

Madhara mengi hutokea ndani ya siku chache za kwanza baada ya kuchanjwa. Chanjo za virusi vya korona zina madhara mengi ya kawaida kuliko chanjo zingine. Kwa kawaida dalili huwa na ukali wa kiwango cha chini hadi kiwango cha wastani na hutoweka baada ya siku chache, lakini watu wengine hupata dalili kali zaidi. Vijana mara nyingi hupata madhara makali zaidi kiasi kuliko watu wenye umri mkubwa.

Watu wengi waliochanjwa huhisi uchungu mahali walipodungwa sindano. Madhara mengine ya kawaida ni pamoja na uchovu, kuumwa na kichwa, maumivu ya misuli, kuhisi baridi, maumivu ya viungo na joto jingi mwilini. Madhara haya ni ya kawaida zaidi baada ya kupokea dozi ya pili.

Si kawaida kupata madhara makali. Madhara yasiyo ya kawaida ni pamoja na kuvimba kwa moyo (kuvimba kwa misuli ya moyo na kuvimba kwa utando unaozunguka moyo). Kwa kawaida madhara haya hutokea baada ya kupokea dozi ya pili na mara nyingi hutokea kwa vijana na watu wenye umri wa makamo. Madhara yasiyo ya kawaida kama vile mizio mikali na kuvimba kwa moyo yanaweza kutibiwa iwapo yatatokea. Hata hivyo, hatuwezi kupuuza suala la kutokea kwa madhara yasiyo ya kawaida au madhara ambayo hutokea tu baada ya kipindi fulani cha kupokea chanjo.

Ninapaswa kufanya nini iwapo nitapata madhara?

Ikiwa utapata dalili zisizotarajiwa, kali au za kudumu, wasiliana na daktari wako au mtoa huduma za afya mwingine ili ufanyiwe uchunguzi na kupata ushauri. Hatua hii ni muhimu bila kujali iwapo unaamini kuwa dalili hizo zinatokana na chanjo au hapana. Watoa huduma za afya wana jukumu la kuripoti dalili zozote kali au zisizotarajiwa ambazo wanashuku kuwa zinatokana na chanjo. Unaweza pia kutuma arifa mwenyewe kupitia tovuti ya helsenorge.no.

Kuidhinishwa kwa masharti

Chanjo hii ya virusi vya korona imefanyiwa majaribio katika tafiti kubwa ambapo maelfu kadhaa ya watu walipokea chanjo hiyo. Tafiti zilifanywa kwa njia sawa na tafiti za chanjo zingine, lakini muda wake wa uchunguzi ulikuwa mfupi. Mamlaka za udhibiti wa dawa zimeidhinisha chanjo hii kwa masharti. Hii inamaanisha kuwa kuna data ya kutosha kutathmini kuwa manufaa ya chanjo ni mengi zaidi kuliko madhara, lakini kuwa ni lazima mtengenezaji wa chanjo aendelee kufanya tafiti na kuendelea kutoa data kwa mamlaka za udhibiti wa dawa wakati inapopatikana.

Nimepokea chanjo gani?

Ukiwa umepokea chanjo ya virusi vya korona, itarekodiwa kwenye Sajili ya Utoaji Chanjo ya Norwe (Norwegian Immunisation Registry), SYSVAK. Unaweza kufikia maelezo yako katika tovuti ya helsenorge.no.

Je, ungependa kupata maelezo zaidi?

Tafadhali mwulize daktari wako au mtoa huduma za afya mwingine au tembelea tovuti ya Taasisi ya Afya ya Norwe (Norwegian Institute of Health) katika fhi.no/cip.